# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU
KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO

# MKAKATI WA KUKUZA KAZI ZA STAHA KWA WAFANYAKAZI WA NYUMBANI 2025/2026 – 2029/2030

**DESEMBA, 2025**

## YALIYOMO


**DIBAJI**............ **III**
**SHUKRANI**............ **IV**
**VIFUPISHO VYA MANENO**............ **V**
**SURA YA KWANZA**............ **1**
**1.0 UTANGULIZI**............ **1**
**1.1** Umuhimu wa Kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa Wafanyakazi wa Nyumbani............ **2**
**1.2** Dira na Dhima............ **3**
**1.2.1** Dira............ **3**
**1.2.2** Dhima............ **3**
**1.3** Lengo Kuu............ **3**
**1.4** Malengo Mahsusi............ **3**
**SURA YA PILI**............ **4**
**WAFANYAKAZI WA NYUMBANI NCHINI**............ **4**
**2.0** Utangulizi............ **4**
**2.1** Tathmini wa Hali Halisi............ **4**
**2.1.1** Ufafanuzi wa Mfanyakazi wa Nyumbani............ **4**
**2.1.2** Uchambuzi wa Takwimu............ **5**
**2.1.3** Mfumo wa Kisera na Kisheria............ **6**
**2.2** Uzoefu kutoka Nchi Nyingine............ **8**
**SURA YA TATU**............ **9**
**UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA WAFANYAKAZI WA NYUMBANI**............ **9**
**3.0** Utangulizi............ **9**
**3.1** Nguzo Muhimu za Kimkakati............ **9**
**3.1.1** Mazingira ya Kazi yenye Staha............ **9**
**3.1.2** Hifadhi ya Jamii na Ustawi............ **9**
**3.1.3** Ulinzi wa Kisheria, Uelewa wa Haki na Wajibu............ **9**
**3.1.4** Kuendeleza Ujuzi na Ukuaji Kitaaluma............ **10**
**3.1.5** Vyama vya Wafanyakazi na Uchechemuzi............ **10**
**3.1.6** Ulinzi wa Wafanyakazi wa Nyumbani Wahamiaji............ **10**
**3.2** Matokeo Tarajiwa, Malengo, Shughuli na Viashiria Muhimu vya Utendaji **11**
**3.2.1** Nguzo Ya 1. Mazingira ya Kazi yenye Staha............ **11**
**3.2.2** Nguzo Ya 2: Hifadhi ya Jamii na Ustawi............ **11**
**3.2.3** Nguzo Ya 3: Ulinzi wa Kisheria, Uelewa wa Haki na Wajibu............ **12**
**3.2.4** Nguzo Ya 4: Kuendeleza Ujuzi na Ukuaji Kitaaluma............ **13**

**3.2.5** Nguzo Ya 5: Vyama vya Wafanyakazi na Uchechemuzi............................ **14**
**3.2.6** Nguzo Ya 6: Ulinzi wa Wafanyakazi wa Nyumbani Wahamiaji.................. **14**
**SURA YA NNE**.................................................................................................. **16**
**MPANGILIO WA TAASISI NA MUUNDO WA URATIBU**.......................................... **16**
**4.0** Utangulizi................................................................................................ **16**
**4.1** Mfumo wa Uratibu..................................................................................... **16**
**4.2** Majukumu na Wajibu wa Wadau.................................................................. **16**
**SURA YA TANO**............................................................................................... **18**
**UFUATILIAJI NA TATHMINI**.............................................................................. **18**
**5.0** Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini.............................................................. **18**
**5.1** Viashiria Muhimu vya Kiutendaji................................................................ **18**
**5.2** Uwasilishaji wa Taarifa na Uwajibikaji....................................................... **18**
**SURA YA SITA**................................................................................................. **19**
**6.0 HITIMISHO**..................................................................................................... **19**
**KIAMBATISHO CHA 1: JEDWALI LA MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**............ **20**

## DIBAJI

Wafanyakazi wa Nyumbani nchini Tanzania huchangia kwa kiasi kikubwa katika ustawi wa kaya, maendeleo ya jamii na ukuaji wa uchumi wa Taifa. Licha ya mchango wao mkubwa, Wafanyakazi wa Nyumbani wameendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu haki zao. Mkakati wa Kitaifa wa Wafanyakazi wa Nyumbani ni hatua ya kushughulikia changamoto hizi kwa kuhakikisha kwamba, Wafanyakazi wa Nyumbani, wanaofanya Kazi ndani na nje ya nchi, wanapewa haki na fursa wanazostahili.

Kama Taifa linalojitahidi kujenga uchumi jumuishi, wa haki na endelevu, tunatambua kuwa kuwawezesha Wafanyakazi wa Nyumbani ni muhimu kwa maendeleo ya jamii kwa ujumla. Malengo yaliyowekwa ndani ya Mkakati huu yanaonesha dhamira yetu ya dhati ya kuwalinda na kuboresha ustawi wa Wafanyakazi wa Nyumbani sambamba na malengo mapana ya usawa wa kijamii na ukuaji wa uchumi. Kupitia uimarishaji wa Mifumo ya Kisheria, upatikanaji wa ulinzi wa kijamii na kukuza maendeleo ya ujuzi wa kitaaluma, Mkakati huu unalenga kuanzisha mazingira imara ambapo Wafanyakazi wa Nyumbani watalindwa na pia watakuwa na fursa ya kustawi.

Mkakati huu unatilia mkazo uimarishaji wa uwezo wa Taasisi na mshikamano wa Wadau mbalimbali kama Serikali, Waajiri, Vyama vya Wafanyakazi na Mashirika ya Kijamii. Kupitia ushirikiano na uwajibikaji wa pamoja, Kazi za Nyumbani zinalengwa kubadilishwa kuwa Sekta yenye Mazingira ya Kazi zenye Staha. Tunadhamiria kuwa utekelezaji wa Mkakati huu utaleta mafanikio yanayoonekena na kupimika. Mabadiliko haya yataleta manufaa si tu kwa Wafanyakazi wa Nyumbani, bali pia kwa Jamii nzima ya Watanzania, huku tukijenga Taifa lenye usawa, heshima na maendeleo kwa wote.

Tunatambua ushiriki wa Wadau wa Kijamii, ikiwemo Vyama vya Waajiri, Vyama vya Wafanyakazi wa Nyumbani, pamoja na Mashirika yasiyo ya Kiserikali ambao wamechangia kwa namna ya kipekee katika kufanikisha kukamilishwa kwa Mkakati huu, hivyo natoa shukrani za dhati kwa wote walioshiriki katika kuandaa Mkakati huu. Tunapoingia katika hatua ya utekelezaji, natoa wito kwa wadau wote kushirikiana kwa karibu na Serikali ili kufanikisha utekelezaji wa Mkakati huu na kutimiza malengo yake kikamilifu na hivyo, kuhakikisha haki na ustawi wa Wafanyakazi wa Nyumbani unalindwa na kuendelezwa kwa maslahi ya Taifa letu.

Mhe. Deus Clement Sangu (Mb)
**WAZIRI WA NCHI - OFISI YA WAZIRI MKUU**
**(KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO)**

**SHUKRANI**

Mkakati wa Kitaifa kwa Wafanyakazi wa Nyumbani umeandaliwa kwa juhudi za pamoja kati ya Serikali, Waajiri, Vyama vya Wafanyakazi, Taasisi na Mashirika yasiyo ya kiserikali kwa nia ya dhati ya kulinda utu, haki na maisha bora ya Wafanyakazi wa Nyumbani. Ni matokeo ya mshikamano na azma ya kweli ya kubadili maisha ya kundi hili muhimu linalochangia ustawi wa familia zetu na Jamii kwa ujumla.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka Mifumo ya Kisheria inayosimamia haki za wafanyakazi ikiwa ni pamoja na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977) katika Ibara ya 22 na 23 inatoa haki ya kufanya kazi na kulipwa ujira bila ubaguzi; Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini Sura 366 ambayo inaweka misingi ya jumla ya ajira nchini pamoja na Sheria ya Taasisi za Kazi Sura 300 ambayo imeweka Mifumo ya Kitaasisi katika kusimamia mahusiano ya kiajira nchini.

Katika kutekeleza Sheria tajwa Serikali imefanya jitihada mbalimbali ili kuhakikisha Wafanyakazi wa Nyumbani wanastawi, jitihada hizo ni pamoja na kuweka mifumo ya kitaasisi inayosimamia masuala ya Wafanyakazi wa Nyumbani kwa kuweka Kima cha Chini cha Mshahara, Kukuza uhuru wa kujumuika katika Vyama vya Wafanyakazi ili wawe na sauti ya pamoja katika kutetea haki zao, usajili wa Mawakala Binafsi wa Ajira ambao huwaunganisha Wafanyakazi wa Nyumbani na waajiri wao, kusainiwa kwa Mikataba ya Makubaliano ya Uwili (*Birateral Agreements*) na nchi nyingine, kuimarisha ushirikiano na Mashirika ya Kimataifa katika kutekeleza Mikataba ya Kimataifa.

Pamoja na jitihada hizo, Mkakati huu unalenga kuimarisha Kazi za Staha kwa Wafanyakazi wa Nyumbani nchini, kupitia maboresho mbalimbali ya kuimarisha ulinzi wa Kisheria, kuwezesha upatikanaji wa Haki kwa kuboresha Kaguzi za Kazi, usimamizi na Utatuzi wa Migogoro ya Kikazi, kuongeza wigo wa fursa za Mafunzo ya kitaalam, kuongeza wigo wa ushirikishwaji wa Wafanyakazi wa Nyumbani katika Vyama vya Wafanyakazi, kukuza wigo wa huduma za Hifadhi ya Jamii na upatikanaji wa Huduma za Afya.

Mary N. Maganga
**KATIBU MKUU – OFISI YA WAZIRI MKUU**
**(KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO)**

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| **ATE** | Chama cha Waajiri Tanzania |
| **CMA** | Tume ya Usuluhishi na Uamuzi |
| **ILO** | Shirika la Kazi Duniani |
| **MoUs** | Hati ya Maelewano |
| **OSHA** | Wakala wa Usalama na Afya Mahali Pa Kazi |
| **PM-RALG** | Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| **OWM-KAM** | Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano |
| **TUCTA** | Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania |
| **TVET** | Elimu ya Mafunzo ya Ufundi Stadi |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Usuli

Nchini Tanzania, Wafanyakazi wa Nyumbani wana jukumu la kipekee katika jamii wakitoa huduma za msingi katika Kaya na kutoa fursa kwa Waajiri wao kuwawezesha kupata nafasi ya kushiriki katika shughuli nyingine za kiuchumi na kijamii. Licha ya mchango wao mkubwa, Wafanyakazi wa Nyumbani wanakabiliwa na mazingira duni ya kazi, kutojua haki zao, mishahara midogo na kukosa Mikataba ya Kazi. Ili kuimarisha mazingira ya kazi yenye Staha upo umuhimu mkubwa wa uwepo wa Mkakati wa Kitaifa wa Wafanyakazi wa Nyumbani ili kushughulikia changamoto zinazowakabili.

Kwa mujibu wa Utafiti wa Watu wenye Uwezo wa Kufanya Kazi wa mwaka 2020/21, asilimia 5.6 ya watu milioni 23.5 walioajiriwa nchini wanafanya Kazi katika Sekta ya Nyumbani, huku wanawake wakiwa asilimia 66.5 ya Wafanyakazi hao. Shirika la Kazi Duniani limebainisha hali ya mazingira magumu ya Wafanyakazi wa Nyumbani na kuweka wazi kuhusu kutotambuliwa rasmi kwa Kazi za Nyumbani katika nchi nyingi, ikiwemo Tanzania.

Idadi kubwa ya Wafanyakazi wa Nyumbani ni wanawake na vijana kutoka maeneo ya Vijijini ambao wanakabiliwa na changamoto mbalimbali katika Soko la Ajira. Wafanyakazi wengi wa Nyumbani wamekuwa wakifanya kazi kwa makubaliano yasiyo rasmi, licha ya Sheria ya Ajira na Uhusiano ya Kazini Sura 366 kulinda haki za Wafanyakazi wote katika Sekta Binafsi. Aidha, pamoja na kuwa na Sheria ya Taasisi za Kazi Sura 300 ambayo imepiga hatua kwa kuwajumuisha Wafanyakazi wa Nyumbani katika utaratibu wa Kima cha Chini cha Mshahara, Wafanyakazi hawa wapo katika hatari ya unyonyaji, unyanyasaji na kufanyishwa kazi kwa masaa mengi[1].

Mwaka 2017 Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilifanya tathmini ya mapungufu ya kisheria kwa kulinganisha na Mkataba wa Shirika la Kazi Duniani Namba 189 wa Wafanyakazi wa Nyumbani. Aidha, mwaka 2022 ilitengeneza Mpango Kazi wa Utatu ili kuhamasisha Kazi zenye Staha kwa Wafanyakazi wa Nyumbani.

Mkakati huu wa Kitaifa kwa Wafanyakazi wa Nyumbani unabaki kuwa muhimu katika kuhakikisha Wafanyakazi wa Nyumbani wanapata ulinzi, kutambuliwa na kuzifikia fursa wanazostahili ili kukuza Kazi za Staha.

[1] Taarifa ya ILO (2017); Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi wa Nyumbani; iliyotolewa tarehe 12 Julai 2017 nchini Tanzania

## 1.1 Umuhimu wa kuandaa Mkakati wa kitaifa wa Wafanyakazi wa Nyumbani

Wafanyakazi wa Nyumbani nchini wana jukumu muhimu katika jamii wakitoa huduma muhimu zinazowezesha familia kushiriki katika kazi na shughuli nyingine za kijamii. Hata hivyo, licha ya mchango wao muhimu, Wafanyakazi hawa wanakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazoathiri ustawi wao. Baadhi ya changamoto hizo ni:

i) **Mshahara mdogo na ucheleweshwaji wa malipo**: Wafanyakazi wengi wa Nyumbani wanalipwa chini ya Kima cha Chini cha Mshahara, huku baadhi yao wakicheleweshwa malipo.

ii) **Ukosefu wa uelewa wa haki zao**: Baadhi ya Wafanyakazi wa Nyumbani hawana uelewa kuhusu haki zao zilizoanishwa katika Sheria za Kazi na hivyo kusababisha kutokuwa na Mazingira ya Kazi yenye Staha.

iii) **Kutokuwa na Mkataba ya Ajira**: Wafanyakazi wa Nyumbani mara nyingi huajiriwa kwa makubaliano yasiyo rasmi, bila Mkataba wa Maandishi unaobainisha masharti ya ajira, hali inayowakosesha haki zao za msingi.

iv) **Kukosekana kwa chombo cha uwakilishi kwa Waajiri wa Wafanyakazi wa Nyumbani:** Kutokuwepo kwa Taasisi rasmi inayowakilisha Waajiri wa Wafanyakazi wa Nyumbani kunakwamisha juhudi za kushughulikia haki za Wafanyakazi. Bila uwakilishi wa pamoja, Waajiri wa Wafanyakazi wa Nyumbani hukosa jukwaa la kutetea maslahi yao na kushiriki katika mijadala ya Sera kwa njia ya usawa.

v) **Wigo mdogo wa Mifumo ya Hifadhi ya Jamii:** Wafanyakazi wengi wa **Nyumbani** hawajumuishwi katika Mifumo ya Hifadhi ya Jamii, hali inayowaacha bila kinga wakati wa dharura za kiafya, uzee au wanapopoteza ajira.

vi) **Wigo mdogo wa ufikiaji wa huduma za Vyama vya Wafanyakazi na Majadiliano ya Pamoja:** Wafanyakazi wengi wa Nyumbani wanakosa fursa ya kujiunga na Vyama vya Wafanyakazi au kushiriki katika Mifumo ya majadiliano ya pamoja ambayo ni njia muhimu za kuboresha hali zao za kazi na kujadili mishahara bora.

vii) **Masaa mengi ya kazi bila mapumziko au malipo ya ziada:** Wengi wa Wafanyakazi wa Nyumbani hufanya kazi kwa masaa mengi, mara nyingi bila kupumzika wala kulipwa kwa kazi ya ziada. Hali hii huathiri ustawi wa maisha yao kwa ujumla.

viii) **Kukabiliana na ukatili, unyanyasaji na udhalilishaji:** Wafanyakazi wengi wa Nyumbani, hususan wanawake na vijana hukabiliwa na manyanyaso ya kimwili na kihisia, pamoja na ukatili wa kingono.

ix) **Wigo mdogo wa Mifumo Usalama na Afya kazini:** Sheria ya Usalama na Afya Mahali Pa Kazi ya mwaka 2003 inatafsiri kwa upana eneo la kazi kama mahali popote mtu anapofanya kazi, ikijumuisha Viwanda, Ofisi na maeneo ya ujenzi. Hata hivyo, Sheria hii haijataja wazi nyumba binafsi, jambo linalowaacha Wafanyakazi wa Nyumbani bila ulinzi wa Kisheria kuhusu usalama wa kazini.

Changamoto hizi zinaonesha hitaji la haraka la kuwa na Mkakati wa Kitaifa ambao si tu unashughulikia matatizo ya sasa, bali unaweka msingi wa suluhisho endelevu kupitia mageuzi ya Kisera, ulinzi wa Kisheria na Mifumo ya utekelezaji. Hivyo, Umuhimu wa kuandaa Mkakati wa Kitaifa kwa Wafanyakazi wa Nyumbani umejengwa juu ya haja ya kurasimisha na kulinda Kazi za Nyumbani kama ajira rasmi, chini ya Sheria na kuweka Mifumo madhubuti ya utekelezaji.

## 1.2 DIRA NA DHIMA

### 1.2.1 Dira

Tanzania yenye Wafanyakazi wa Nyumbani waonajivunia kufanya Kazi zenye Staha.

### 1.2.2 Dhima

Kuhakikisha haki na mazingira bora kwa Wafanyakazi wa Nyumbani yanaimarishwa kupitia maboresho ya Kisheria na utekelezaji wa misingi ya Kazi yenye Staha.

## 1.3 Lengo kuu

Kuimarisha Kazi za Staha kwa Wafanyakazi wa Nyumbani nchini.

## 1.4 Malengo Mahsusi

**i)** Kuimarisha ulinzi wa Kisheria na kutekeleza Sera zinazohakikisha Wafanyakazi wa Nyumbani wananufaika na Viwango vya Ajira na Haki za Kisheria;

**ii)** Kuimarisha Taasisi na kuwezesha upatikanaji wa haki kwa kuboresha Kaguzi za Kazi, usimamizi na Utatuzi wa Migogoro ya Kikazi kupitia Ofisi za Kazi na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi;

**iii)** Kuongeza wigo wa fursa za Mafunzo kwa Wafanyakazi wa Nyumbani ili kuwajengea uwezo wa kitaaluma na kuwahakikishia usalama wa ajira;

**iv)** Kuimarisha wigo ushirikishwaji wa Wafanyakazi wa Nyumbani katika Vyama vya Wafanyakazi, uhamasishaji na Kampeni za uchechemuzi kuhusu haki za Wafanyakazi wa Nyumbani na wajibu wa Waajiri;

**v)** Kukuza wigo wa huduma za Hifadhi ya Jamii na upatikanaji wa huduma za afya kwa kuhakikisha Wafanyakazi wa Nyumbani wanapata huduma za matibabu, Bima za Afya na Mafao ya Uzee.

## SURA YA PILI

## WAFANYAKAZI WA NYUMBANI NCHINI

### 2.0 Utangulizi

Katika jitihada za kuhakikisha utambuzi rasmi, uhalali wa ajira na ulinzi wa haki za Wafanyakazi wa Nyumbani nchini, Mwaka 2012, Shirika la Kazi Duniani lilifanya Tathmini ya kina ya hali ya Wafanyakazi wa Nyumbani. Tathmini hiyo ililenga kuweka msingi wa kukuza mazingira ya kazi yenye usawa, heshima na staha kwa kundi hili. Kwa kutambua nafasi ya kipekee ya Wafanyakazi wa Nyumbani katika jamii ya Watanzania ikiwajumuisha walezi wa watoto; wapishi; wafanya usafi; wasaidizi wa kazi za ndani; na kwa kiasi kikubwa wasimamizi wa kaya katika familia, Taarifa ya Tathmini ilibainisha kuwa “sekta rasmi” yenye ulinzi wa kisheria haingeweza kuendelea kwa ufanisi bila mchango wa kundi hili. Aidha, madhara ya kutoimarishwa kwa Sekta ya Wafanyakazi wa Nyumbani yangeweza kuathiri Ufanisi wa Sekta rasmi na hatimaye kuathiri uchumi wa Taifa kwa ujumla. Taarifa hiyo pia ilitoa uchambuzi wa mchango wa Wafanyakazi wa Nyumbani katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi, ikieleza hatua zilizopigwa hadi sasa pamoja na changamoto zinazozuia upatikanaji wa ajira yenye staha kwao.[2]

### 2.1 Tathmini ya Hali halisi

#### 2.1.1 Ufafanuzi wa Mfanyakazi wa Nyumbani

Kumekuwa na mitazamo mbalimbali kuhusu tafsiri sahihi ya "Mfanyakazi wa Nyumbani" hapa nchini. Hali hii inaonesha kuwepo kwa mkanganyiko katika Mfumo wa Kisheria wa sasa kuhusu nani anapaswa kutambuliwa kama Mfanyakazi wa Nyumbani, jambo linaloathiri jitihada za kuwalinda ipasavyo. Ingawa Wafanyakazi wa Nyumbani wanajumuishwa katika Sheria za Kazi, matumizi ya tafsiri pana na jumuishi ya Kazi za Nyumbani ndani ya Sheria hizo kunachangia kuchanganya mipaka ya nani hasa anastahili kutambuliwa rasmi kama Mfanyakazi wa Nyumbani.

Kwa mujibu wa Utafiti ulioainishwa katika taarifa ya Shirika la Kazi Duniani ya mwaka 2016, Wafanyakazi wa Nyumbani nchini hufanya kazi mbalimbali kama vile: kusafisha nyumba, kupika, kufua na kunyoosha nguo, kulea watoto, kuwatunza wazee au wagonjwa, kulima bustani, kulinda nyumba, kuwa dereva wa familia na hata kuwahudumia wanyama wanaofugwa nyumbani.

---

[2] Ripoti ya ILO (2016); Uchambuzi wa Hali ya Wafanyakazi wa Nyumbani katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Ofisi ya Nchi, Dar es salaam.

### 2.1.2 Uchambuzi wa Takwimu

#### i) Tathmini ya hali ya Wafanyakazi wa Nyumbani (2016);

Tathmini ya Hali ya Wafanyakazi wa Nyumbani iliyofanywa na Shirika la Kazi Duniani hapa nchini ilibainisha kuwepo kwa Wafanyakazi wa Nyumbani wapatao 883,779 kwa Tanzania Bara na 203,622 kwa Zanzibar waliokuwa katika ajira rasmi. Idadi hii iliwakilisha asilimia 5 ya watu wote wanaofanya kazi katika kundi la umri wa miaka 15–64. Hata hivyo, tathmini hiyo ilionesha kuwa iwapo Wafanyakazi wa Nyumbani walioko kwenye ajira zisizo rasmi wangekadiriwa pia, idadi ya jumla ingeongezeka hadi kufikia 1,728,228, sawa na asilimia 7 ya nguvu kazi yote ya Taifa, kwa kuzingatia makadirio ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012.

#### ii) Kazi za Nyumbani zisizo na ujira nchini Tanzania (2016);

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa asilimia 54 ya Kazi za Nyumbani nchini Tanzania hazikuwa zenye ujira. Sehemu kubwa ya kazi hizo hufanywa na wanafamilia kama vile mabinti wa familia na ndugu wa karibu, sambamba na Wafanyakazi wa Nyumbani wanaolipwa. Kukosekana kwa taratibu rasmi katika ajira za Kazi za Nyumbani kulishamiri, kwani mahusiano kati ya Mwajiri na Mfanyakazi mara nyingi yalionekana kama msaada wa kifamilia au wa kijamii badala ya ajira rasmi.

#### iii) Takwimu za Kazi za Nyumbani Duniani za mwaka 2024:

Muhtasari wa Kisera ulioandaliwa na Shirika la Kazi Duniani uliopewa jina la “Kutoka kwenye Mgogoro wa Huduma za Malezi Ulimwenguni hadi Huduma Bora za Malezi Majumbani”, uliotolewa Machi 2024, inakadiriwa kuwa duniani kote kuna takribani Wafanyakazi wa Nyumbani milioni 75.6 wenye umri wa miaka 15 na zaidi. Hii ni pamoja na wanaoajiriwa moja kwa moja na Kaya Binafsi na wanaofanya kazi kupitia watoa huduma. Wanawake wanawakilisha asilimia 76.2 ya Wafanyakazi hao na Kazi za Nyumbani huchangia asilimia 4.5 ya ajira ya wanawake duniani.

#### iv) Kazi ya Nyumbani nchini Tanzania (2020/21):

Utafiti wa Watu wenye Uwezo wa Kufanya Kazi wa mwaka 2020/21 ulibainisha kuwa asilimia 5.6 ya watu milioni 23.5 walioko kwenye ajira nchini walifanya kazi katika sekta ya Kazi za Nyumbani. Wanawake walikuwa asilimia 66.5 ya Wafanyakazi wote wa sekta hiyo. Takwimu hizi zinaendana na mwelekeo wa Kimataifa, ambapo wengi wa Wafanyakazi wa Nyumbani nchini ni wanawake na vijana kutoka maeneo ya vijijini, ambao hukumbana na changamoto nyingi katika soko la ajira.

**v) Hatua zilizochukuliwa na Serikali kuhusu Haki za Wafanyakazi wa Nyumbani (Baada ya mwaka 2016):**

Baada ya matokeo hayo, Serikali ya Tanzania imechukua hatua mbalimbali za kuboresha haki na mazingira ya kazi ya Wafanyakazi wa Nyumbani. Hata hivyo, changamoto bado zipo, kutokana na kuendelea kuwepo kwa ajira zisizo rasmi katika Kazi za Nyumbani na kazi hizo kutotambuliwa kama ajira rasmi. Serikali inaendelea kushughulikia changamoto hizi kupitia Sera na Mifumo ya ulinzi wa kazi.

### 2.1.3 Mfumo wa Kisera na Kisheria

Kushughulikia mapungufu ya kufikia kazi zenye Staha ni ngumu pale ambapo kazi husika zinafanyika nje ya Mfumo rasmi wa Kisheria. Kwa kuzingatia hilo, Kamati ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni ilieleza katika taarifa yake ya mwaka 2006 (aya ya 10) kuwa Kazi za Nyumbani zinapaswa kuwa chini ya udhibiti wa Sheria za Kitaifa zinazozingatia Viwango vya Kimataifa, ili kuhakikisha Wafanyakazi wa Nyumbani wanalindwa sawa na Wafanyakazi wengine katika Sekta rasmi. Zifuatazo ni baadhi ya Sheria na Kanuni muhimu zinazohusiana na Kazi za Nyumbani:

**i) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977)**

Ibara ya 13(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaeleza kuwa watu wote ni sawa mbele ya Sheria na wanastahili kulindwa bila ubaguzi wowote. Aidha, Ibara ya 23(1) inabainisha kuwa kila mtu anayo haki ya kulipwa ujira unaolingana na kazi anayoifanya, bila ubaguzi wowote. Kwa kuzingatia misingi ya Ibara tajwa, Serikali imetambua umuhimu wa kuandaa Mkakati mahsusi wa kuimarisha utambuzi, uhalalishaji na ulinzi wa haki za Wafanyakazi wa Nyumbani kama sehemu ya utekelezaji wa Katiba.

**ii) Sheria za Kitaifa**

Tangu mwaka 2016, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limeendelea kufanya marekebisho, kufuta na kutunga Sheria mbalimbali zenye lengo la kuimarisha ulinzi wa Kisheria kwa Wafanyakazi wa Nyumbani nchini. Baadhi ya Sheria muhimu zinazohusiana moja kwa moja na haki na ulinzi wa Wafanyakazi wa Nyumbani ni kama ifuatavyo:

**a) Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini, Sura 366**

Sheria hii inaweka misingi ya jumla ya ajira nchini, ikijumuisha haki mbalimbali za Wafanyakazi kama vile Mikataba ya Kazi, Masaa ya Kazi, Likizo n.k. Kwa ujumla Sheria hii inawahusu Wafanyakazi wote ikiwemo Wafanyakazi wa Nyumbani. Wafanyakazi wa Nyumbani wanajumuishwa katika Sheria hii licha ya kuwepo baadhi ya mapungufu katika utekelezaji.

**b) Sheria ya Taasisi za Kazi, Sura 300**

Sheria hii imeweka Mifumo ya Kitaasisi katika kusimamia mahusiano ya kikazi nchini. Inajumuisha taratibu za Kaguzi za Kazi utatuzi wa Migogoro ya Kazi na Ushirikishwaji wa Wafanyakazi katika maeneo ya kazi. Mifumo hii imewatambua Wafanyakazi wa Nyumbani licha ya changamoto ya Kaya kutotambulika kama maeneo ya kazi.

**c) Sheria ya Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432**

Sheria hii inashughulikia suala la usafirishaji haramu wa binadamu, pamoja na usafirishaji kwa ajili ya ajira za nyumbani. Inatoa msingi wa Kisheria wa kuzuia usafirishaji, kuwalinda waathirika na kuwachukulia hatua wahusika.

**iii) Sera za Kitaifa**

Serikali imeendelea kuhamasisha Kazi za Staha kwa Wafanyakazi wote ikiwemo Wafanyakazi wa Nyumbani kupitia Sera mbalimbali zilizoundwa. Miongoni mwa Sera hizi ni pamoja na: Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008, Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya mwaka 2023, Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008, Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 na Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2023. Sera hizi kwa pamoja zinatoa Mwongozo wa kukuza ajira kwa vijana, kukuza ujuzi unaohitajika kwa Watanzania wanaotafuta ajira na kubadilisha sekta isiyo rasmi ili kuzalisha ajira zenye Staha.

iv) **Mipango ya Kitaifa**

Serikali imekuwa ikitekeleza Mipango mbalimbali ya Kitaifa ikiwemo Dira ya Maendeleo ya Taifa (2050)**,** Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026)**,** Mpango wa Kitaifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (2024/2025 – 2028/2029) na Mkakati wa Pili wa Taifa wa Kutokomeza Utumikishwaji wa Mtoto (2024/25 - 2028/29). Mipango hii pamoja mambo mengine inalenga kukuza haki na ustawi wa Wafanyakazi wote nchini wakiwemo Wafanyakazi wa Nyumbani.

**v) Programu na Miradi iliyoanzishwa**

Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo na Mashirika yasiyo ya Kiserikali, imekuwa ikitekeleza Miradi mbalimbali tangu mwaka 2016 kwa ajili ya kuboresha utambuzi na mazingira ya kazi kwa Wafanyakazi wa Nyumbani nchini. Miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa ***Improving dercent Work for Domestic Workers*** ambao unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na wadau wa Utatu; Programu za Mafunzo endelevu zinazoendeshwa na Chama cha Wafanyakazi wa Nyumbani na Sekta isiyo Rasmi Tanzania chini ya Mradi wa *EmPoWeReD* II**;** Mradi wa "Upatikanaji wa Haki na Kuzuia Vitendo vya Ukatili wa Kijinsia kwa

Wafanyakazi wa Nyumbani", unaoendeshwa na *Light for Domestic Workers (*LDW*)* kwa kushirikiana na *Women Fund Trust - Tanzania* (WFT-T). Miradi hii inaonyesha dhamira ya nchi katika kuboresha ustawi wa Wafanyakazi wa Nyumbani.

Aidha, Miradi hii inatekeleza Mikataba ya ILO ikiwemo; Mkataba Na. 189 kuhusu Wafanyakazi wa Nyumbani (2013)**,** Mkataba Na. 87 na 98 kuhusu haki za Wafanyakazi (1964)**,** pamoja na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kuondoa Aina zote Ubaguzi Dhidi ya Wanawake wa mwaka (CEDAW- 1979), ambayo inalinda haki na ustawi Wafanyakazi wa Nyumbani.

### 2.2 Uzoefu kutoka Nchi nyingine

Katika nchi mbalimbali duniani, kumekuwa na mwelekeo wa kuimarisha ulinzi wa haki za Wafanyakazi wa Nyumbani kupitia Sera na Sheria mahsusi. Uchambuzi ufuatao unaangazia hali ya Ajira za Nyumbani katika nchi mbili (2), ukielezea changamoto zilizopo na mafanikio katika kuboresha Sekta ya kazi za Nyumbani [3]:

i) **Afrika Kusini:** Wafanyakazi wa Nyumbani wanatambuliwa chini ya Sheria za Kazi, wakilindwa dhidi ya ujira wa chini, muda wa kazi na hifadhi ya kijamii. Hata hivyo, utekelezaji wa Sheria hizi ni changamoto kubwa, hasa katika maeneo ya Vijijini. Licha ya changamoto hiyo, nchi hii imepiga hatua kwa kuweka Mifumo thabiti ya kushughulikia masuala ya Utatuzi wa Migogoro ya Kazi kwa Wafanyakazi wa Nyumbani.

ii) **Zambia**: Nchi hii imepiga hatua kubwa katika kurasimisha Ajira za Nyumbani kwa kuhakikisha Wafanyakazi wanapata ulinzi mahususi wa ajira. Hata hivyo, bado kuna changamoto kuhusu utekelezaji wa Mikataba na malipo ya haki, hivyo nchi iliandaa Mkakati ulitwa Mpango wa Kitaifa kwa Kazi za Nyumbani Zambia wa Mwaka 2015-2021 (National Plan of Action for Domestic Work in Zambia of 2015- 2021) kwa ajili ya kutatua changamoto hiyo.

Uzoefu huu unaonesha kuwa hata pale ambapo Mifumo ya Kisheria ipo, utekelezaji na ushirikishwaji kamili wa Wafanyakazi wa Nyumbani bado ni changamoto jambo linaloibua haja ya kuwa na Mikakati jumuishi, inayotekelezeka na yenye usimamizi madhubuti.

[3] Shirika la Kazi Duniani (2021); *Ulinzi wa Haki za Wafanyikazi wa Majumbani: Muhtasari wa Kimataifa wa Sera na Changamoto*. Shirika la Kazi Duniani. https://www.ilo.org/global/publications

# SURA YA TATU

## UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA WAFANYAKAZI WA NYUMBANI

## 3.0 Utangulizi

Sura hii inaeleza Nguzo Kuu za Kimkakati, Matokeo yanayokusudiwa, Malengo Mahsusi, Shughuli zitakazotekelezwa, Matokeo yanayotarajiwa, pamoja na Viashiria vya Msingi vya kupima matokeo.

### 3.1 Nguzo muhimu za Kimkakati

#### 3.1.1 Mazingira ya Kazi yenye Staha

Nguzo hii inalenga kuhakikisha kuwa Wafanyakazi wa Nyumbani wanaheshimiwa, wanalipwa ujira stahiki na wanafanya kazi katika mazingira salama na kiutu, kama yalivyoainishwa katika Ibara ya 14 ya Mkataba Namba 189 wa Shirika la Kazi Duniani kuhusu Kazi yenye Staha kwa Wafanyakazi wa Nyumbani.

#### 3.1.2 Hifadhi ya Jamii na Ustawi

Kuwajumuisha Wafanyakazi wa Nyumbani katika Mifumo ya Kitaifa ya Hifadhi ya Jamii ni jambo la muhimu katika kuhakikisha haki na ustawi wao mahali pa kazi. Nguzo hii inalenga kuhakikisha kuwa Wafanyakazi wa Nyumbani wanasajiliwa kikamilifu katika mipango ya Hifadhi ya Jamii kama vile huduma za afya na Mifuko ya Pensheni, kuwezeshwa kwa upatikanaji wa huduma za afya na huduma za msaada wa kifedha; kuanzishwa kwa huduma za dharura kwa Wafanyakazi wa Nyumbani manusura wa ukatili na unyonywaji; kusisitiza umuhimu wa Waajiri kuchangia katika Mafao ya Hifadhi wa Jamii ya Wafanyakazi wa Nyumbani, pamoja na kuimarisha huduma za afya ya akili na ustawi zinazozingatia mahitaji yao mahsusi.

#### 3.1.3 Ulinzi wa Kisheria, uelewa wa Haki na Wajibu

Katika kuendeleza muundo wa nguzo hii, Mikakati ya Kitaifa inapaswa kuhakikisha kuwa Kazi za Nyumbani zinatambuliwa rasmi ndani ya Sheria za Ajira za Kitaifa na pia zinalingana na Viwango vya Kazi vya Kimataifa kama vile Mkataba Na. 189 wa Shirika la Kazi Duniani. Mikakati hiyo pia inapaswa kuimarisha Mifumo ya Kisheria inayoshughulikia Utatuzi wa Migogoro na kulinda haki za Wafanyakazi; kufanya Kampeni za kuelimisha Umma ili kukuza heshima kwa Wafanyakazi wa Nyumbani na kutambua haki zao; kuhamasisha utoaji wa huduma za msaada wa Kisheria kwa Wafanyakazi wa Nyumbani manusura wa ukatili, unyonyaji au waliofukuzwa kazi bila kufuata utaratibu; kuweka Kanuni maalum za maadili kwa ajili ya Wafanyakazi wa Nyumbani; na kuimarisha Mifumo ya Kaguzi za Kazi ili kuhakikisha kuwa haki za Wafanyakazi wa Nyumbani zinazotambulika Kisheria, zinalindwa na kutekelezwa ipasavyo.

### 3.1.4 Kuendeleza Ujuzi na Ukuaji kitaaluma

Kupata nafasi katika Programu za Mafunzo ya Ufundi Stadi zilizopangwa vizuri ni jambo muhimu katika kuhakikisha Wafanyakazi wa Nyumbani wanapata ajira yenye uhakika na kipato bora (ILO, 2012). Kwa mantiki hiyo, kuwekeza katika kukuza ujuzi na kuendeleza taaluma za Wafanyakazi wa Nyumbani ni hatua muhimu inayosaidia katika kuhakikisha ustawi wa kiuchumi na ukuaji wa kazi zao. Nguzo hii imelenga kuwezesha kuanzishwa kwa Programu za Mafunzo ya Ufundi Stadi zilizothibitishwa au zilizoanzishwa mahususi kwa ajili ya kuwajengea uwezo Wafanyakazi wa Nyumbani katika maeneo kama vile huduma ya malezi, kazi za usafi nyumbani na nyanja nyingine maalum zinazohusiana moja kwa moja na kazi zao.

Mafanikio ya hatua hii yanategemea ushirikiano wa karibu na Taasisi za Mafunzo ya Ufundi na Ufundi Stadi (*Technical and Vocational Education and Training* - TVET). Aidha, ni muhimu kuhakikisha kuwa ujuzi au vipaji ambavyo Wafanyakazi wa Nyumbani wamevipata nje ya Mfumo rasmi wa Elimu na Mafunzo vinatambuliwa rasmi. Hili linaweza kutekelezwa kupitia Programu za Utambuzi wa Ujuzi wa Awali (*Recognition of Prior Learning* – RPL) kwa kushirikiana na Vituo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi (*Vocational Education and Training* – VET Centers).

### 3.1.5 Vyama vya Wafanyakazi na Uchechemuzi

Wafanyakazi wa Nyumbani, kama Wafanyakazi wengine, wanastahili kufurahia haki za kujiunga katika Mashirikisho na Vyama vya Wafanyakazi ili kupata nguvu ya pamoja inayohitajika kwa mazungumzo ya pamoja na utetezi. Kwa kuwa Wafanyakazi wa Nyumbani ni miongoni mwa makundi yaliyo hatarini zaidi ya Wafanyakazi wengine, utaratibu madhubuti wa Kisheria ili kudhibiti unyanyasaji katika mazingira yao ya kazi. Katika muktadha huu nguzo hii, inahamasisha Wafanyakazi wa Nyumbani kupewa mazingira bora ya kuweza kuunda au kujiunga na Vyama vya Wafanyakazi, kuwa na uwakilishi katika vyombo vya kufanya maamuzi.

### 3.1.6 Ulinzi wa Wafanyakazi wa Nyumbani Wahamiaji

Ulinzi wa Wafanyakazi wa Nyumbani Wahamiaji ni jambo muhimu ili kuhakikisha wanaweza kuzoea na kuendana na mazingira mapya ya kazi. Nguzo hii inalenga katika kuhimiza Mafunzo kabla ya kuondoka (Pre-departure Training) na mara baada ya kuwasili; kuhakikisha Uingiwaji wa Mikataba ya pande mbili kati ya nchi zinazotuma na zinazopokea Wafanyakazi wa Nyumbani; kudhibiti na kutambua Wakala wa Ajira na Mashirika ya Uajiri; kuimarisha Mifumo ya Usuluhishi wa Migogoro katika ngazi ya ndani; kushirikishan na Viongozi wa Serikali za Mitaa na Viongozi wa Dini na Kisiasa ili kuhakikisha wafanyakazi wanatendewa haki na kuunganishwa na Mamlaka za wenyeji; pamoja na kuimarisha Mifumo ya kushirikiana taarifa ikiwemo mbinu za kutunza takwimu.

## 3.2 Matokeo tarajiwa, malengo, shughuli na viashiria muhimu vya utendaji

### 3.2.1 Nguzo ya 1. Mazingira ya Kazi yenye Staha

***Matokeo tarajiwa ya 1:*** Kuboresha mazingira ya kazi kwa Wafanyakazi wa Nyumbani.

**Malengo ya Kimkakati**

**i)** Mfumo wa Kima cha Chini cha Mshahara kwa Wafanyakazi wa Nyumbani umeanza kutumika; na

**ii)** Mikataba ya viwango vya ajira kwa Wafanyakazi wa Nyumbani iwe imeandaliwa na kutekelezwa.

**Shughuli**

**i.** Kuandaa Warsha za wadau wa Utatu (Serikali, Waajiri na Wafanyakazi) kwa ajili ya kuandaa Mikataba ya Viwango vya Ajira kwa ajili ya Wafanyakazi wa Nyumbani;

**ii.** Kufanya Programu za uhamasishaji kwa Waajiri kila robo mwaka;

**iii.** Kuwezesha Ukaguzi wa pamoja wa kazi kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

**iv.** Kufanya Mapitio ya Mwongozo wa Kaguzi za Kazi ili kujumuisha Fomu mahsusi ya Ukaguzi (Checklist) kwa Wafanyakazi wa Nyumbani;

**v.** Kufanya mapitio ya Kima cha Chini cha Mshahara; na

**vi.** Kuelimisha Waajiri kuhusu haki za Watu Wenye Ulemavu.

**Matokeo**

**i.** Kima cha Chini cha Mshahara kwa Wafanyakazi wa Nyumbani kimewekwa rasmi;

**ii.** Fomu mahsusi ya Ukaguzi (Checklist) Ukaguzi wa Kazi kwa Wafanyakazi wa Nyumbani ipo na inatumika; na

**iii.** Mikataba ya viwango vya ajira kwa Wafanyakazi wa Nyumbani.

**Viashiria muhimu vya kiutendaji**

**i.** Idadi ya Wafanyakazi wa Nyumbani wanaopokea Mshahara usiopungua Kima cha Chini kilichowekwa;

**ii.** Uwiano wa Waajiri wanaozingatia Viwango vya Kazi dhidi ya wale wasiozingatia (compliance vs non-compliance); na

**iii.** Idadi ya waajiri walioelimishwa kuhusu haki za Watu Wenye Ulemavu.

### 3.2.2 Nguzo ya 2: Hifadhi ya jamii na ustawi

***Matokeo tarajiwa ya 2*****:** Kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma za Hifadhi ya Jamii na ustawi kwa Wafanyakazi wa Nyumbani.

**Malengo ya Kimkakati:**

i. Uandikishaji wa Wafanyakazi wa Nyumbani katika Mifumo ya Hifadhi ya Jamii kuongezeka kwa asilimia 2 ifikapo mwaka 2030; na
ii. Kuongezeka kwa uelewa wa Wafanyakazi wa Nyumbani kuhusu Hifadhi ya Jamii.

**Shughuli:**

i. Kuwezesha usajili wa Wafanyakazi wa Nyumbani katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii;
ii. Kufanya uchambuzi wa hali halisi kuhusu ushiriki wa Wafanyakazi wa Nyumbani katika Mifumo ya Hifadhi ya Jamii; na
iii. Kufanya mapitio ya Mfumo wa Fidia kwa Wafanyakazi ili kujumuisha Waajiri wa Wafanyakazi wa Nyumbani.

**Matokeo:**

i. Wafanyakazi wa Nyumbani wamesajiliwa katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii;
ii. Uwepo wa Mfumo wa gharama nafuu katika Hifadhi ya Jamii; na
iii. Wafanyakazi wa Nyumbani wananufaika na Mfuko wa Fidia kwa madhara au majeraha yanayotokea wakati wa utekelezaji wa kazi zao.

**Kiashiria muhimu cha kiutendaji:**

i. Idadi ya Wafanyakazi wa Nyumbani waliosajiliwa katika Mifumo ya Hifadhi ya Jamii.

### 3.2.3 Nguzo ya 3: Ulinzi wa Kisheria, uelewa wa haki na wajibu

***Matokeo tarajiwa ya 3*:** Kuimarika kwa ulinzi wa Kisheria na utekelezaji wa haki za kikazi kwa Wafanyakazi wa Nyumbani.

**Malengo ya kimkakati:**

i. Upatikanaji wa huduma mahsusi za msaada wa Kisheria zinazowalenga Wafanyakazi wa Nyumbani ifikapo 2030; na
ii. Uwepo wa Mfumo wa kushughulikia Migogoro ya Kazi na unaoweza kufikiwa kwa urahisi na Wafanyakazi wa Nyumbani wakiwemo wenye ulemavu pamoja na Waajiri wao, bila vikwazo vya gharama, umbali au urasimu ifikapo mwaka 2030.

**Shughuli:**

i. Kufanya Maboresho ya Sheria za Kazi ili kujuimuisha masuala ya Wafanyakazi wa Nyumbani;
ii. Kufanya Kampeni za uhamasishaji kote nchini kuhusu haki za Wafanyakazi; na
iii. Kuandaa Kanuni maalum za maadili ya utendaji au Kanuni za udhibiti kwa ajili ya Wafanyakazi wa Nyumbani; na
iv. Kutoa huduma za Kliniki inayotembea kwa ajili ya Utatuzi wa Migogoro ya Kazi.

**Matokeo:**

i. Maboresho katika Sheria za Kazi kwa Wafanyakazi wa Nyumbani yamefanyika kufikia 2030;
ii. Mazingira Bora ya Kazi yaliyo rafiki na yenye kulinda haki;
iii. Mifumo ya kufuatilia utekelezaji wa Sheria za Kazi;
iv. Utoaji wa taarifa muhimu kuhusu haki za Wafanyakazi; na
v. Mifumo ya malalamiko inayowajumuisha Wafanyakazi Wenye Ulemavu.

**Viashiria muhimu vya kiutendaji:**

i. Idadi ya malalamiko yaliyopelekwa OWM-KAM
ii. Idadi ya maagizo ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Sheria yaliyotolewa;
iii. Idadi ya Waajiri waliopata uhamasishaji kuhusu haki za Wafanyakazi wa Nyumbani; na
iv. Idadi ya Migogoro ya Kazi iliyowasilishwa kwa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi.

**3.2.4 Nguzo ya 4:** Kuendeleza ujuzi na ukuaji kitaaluma

***Matokeo tarajiwa ya 4:*** Kuimarika kwa umahiri wa Wafanyakazi wa Nyumbani na maendeleo ya kazi zao.

**Lengo la Kimkakati:**

i. Programu za Mafunzo mahsusi kuandaliwa na kutekelezwa ifikapo mwaka 2030.

**Shughuli:**

i. Kuanzisha Programu za Mafunzo ya Ufundi Stadi, Kozi za Cheti na Mafunzo ya Stadi za Maisha zinazozingatia mahitaji ya Watu Wenye Ulemavu;
ii. Kuimarisha uwezo wa Maafisa Kazi na Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi kuhusu marekebisho ya Sheria za kazi;
iii. Kufanya ufuatiliaji wa Wahitimu wa Mafunzo ya Kazi za Nyumbani (tracer study); na
iv. Kutekeleza Programu za kutambua Ujuzi uliopatikana nje ya Mfumo rasmi kwa kushirikiana na Vituo vya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

**Matokeo:**

i. Kuongezeka kwa upatikanaji wa Programu za kukuza Ujuzi na utambuzi wa umahiri wa Wafanyakazi wa Nyumbani; na
ii. Taarifa ya ufuatiliaji wa Wahitimu wa Mafunzo (*tracer report*).

**Viashiria muhimu vya kiutendaji:**

i. Idadi ya Programu zilizoundwa za Mafunzo kwa Wafanyakazi wa Nyumbani na zinazojumuisha Wafanyakazi wa Nyumbani Wenye Ulemavu; na
ii. Idadi ya Wafanyakazi wa Nyumbani waliomaliza Mafunzo ya Ujuzi kwa mafanikio wakiwemo Wenye Ulemavu.

### 3.2.5 Nguzo ya 5: Vyama vya Wafanyakazi na Uchechemuzi

***Matokeo tarajiwa ya 5*****:** Kuimarika kwa ushiriki wa Wafanyakazi wa Nyumbani katika Vyama vya Wafanyakazi.

**Lengo la Kimkakati:**

Kukuza uhuru wa Wafanyakazi wa Nyumbani kujiunga kwenye Vyama vya Wafanyakazi.

**Shughuli:**

i. Kuimarisha ulinganifu na ujumuishaji wa Mifumo ya usimamizi wa Taarifa za Wafanyakazi wa Nyumbani;
ii. Kuandaa Mipango ya Utekelezaji ya kila mwaka kwa ajili ya uchechemuzi;
iii. Kuratibu ushirikiano kati ya Taasisi mbalimbali ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa Sera kupitia Mikutano ya uratibu iliyo rasmi na Vikosi Kazi; na
iv. Kuwezesha Kampeni za utetezi na uhamasishaji kwa ajili ya Wafanyakazi wa Nyumbani.

**Matokeo:**

i. Kuanza kufanya kazi kwa Mifumo ya usaidizi kwa Wafanyakazi wa Nyumbani;
ii. Mipango ya utekelezaji ya kila mwaka imeandaliwa;
iii. Vikao vya Vikosi Kazi vinafanyika; na
iv. Mifumo inayosomana ya usimamizi wa Taarifa na Takwimu.

**Viashiria muhimu vya Kiutendaji:**

i. Idadi ya Wafanyakazi wa Nyumbani waliojiunga na Vyama vya Wafanyakazi;
ii. Idadi ya Majukwaa ya Kidijitali yaliyoanzishwa na yanafanya kazi;
iii. Idadi ya Kampeni za utetezi zilizoanzishwa na kutekelezwa; na
iv. Kupungua kwa utofauti/kukinzana kwa Takwimu.

### 3.2.6 Nguzo ya 6: Ulinzi wa Wafanyakazi wa Nyumbani Wahamiaji

***Matokeo tarajiwa ya 6*****:** Kuimarika kwa ulinzi wa Wafanyakazi wa Nyumbani Wahamiaji.

**Lengo la Kimkakati:**

**i.** Kuimarisha haki za Wafanyakazi wa Nyumbani Wahamiaji ifikapo mwaka 2030.

**Shughuli:**

**i.** Kuandaa na kutekeleza Mifumo ya kuwalinda Wafanyakazi wa Nyumbani Wahamiaji, ikiwa ni pamoja na taratibu salama za uhamaji, nyaraka halali za Kisheria na msaada wa Kidiplomasia kwa Wafanyakazi walioko nje ya nchi;

**ii.** Kuwezesha ushirikiano wa mipakani ili kuhakikisha ulinzi wa Wafanyakazi wa Nyumbani Wahamiaji na kuhimiza ajira zinazozingatia haki katika ngazi ya Kimataifa;

**iii.** Kutoa Mafunzo ya awali kabla ya kusafiri kwa Wafanyakazi wa Nyumbani; na

**iv.** Kuendesha Mafunzo ya kujenga uwezo kwa wadau wanaohusika na haki za Wafanyakazi wa Nyumbani Wahamiaji.

**Matokeo:**

**i.** Kuimarishwa kwa Mifumo ya ulinzi wa Wafanyakazi wa Nyumbani Wahamiaji;

**ii.** Kufanyika kwa Mafunzo ya awali kabla ya kusafiri; na

**iii.** Kuhamasika kwa wadau wa Wafanyakazi wa Nyumbani kuhusu haki za Wafanyakazi wa Nyumbani.

**Viashiria muhimu vya kiutendaji:**

**i.** Kiwango cha ufuatiliaji wa utekelezaji wa Sheria za Kazi;

**ii.** Idadi ya Wafanyakazi wa Nyumbani waliopata Mafunzo;

**iii.** Idadi ya Mikataba au makubaliano ya uwili (*Bilateral Agreements/MoUs*) iliyotiwa saini; na

**iv.** Idadi ya malalamiko ya Wafanyakazi Wahamiaji yaliyoripotiwa katika Ubalozi.

## SURA YA NNE

## MPANGILIO WA TAASISI NA MUUNDO WA URATIBU

### 4.0 Utangulizi

Utekelezaji wenye mafanikio wa Mkakati huu unahitaji ushiriki wa Wadau mbalimbali waliobainishwa kwa majukumu na wajibu wao kwa uwazi. Miongoni mwa wadau hawa ni Serikali, Sekta Binafsi, Taasisi za Kiraia na wadau wa Kijamii na Kiuchumi. Ili kuhakikisha utekelezaji mzuri na wa pamoja wa Mkakati huu miongoni mwa Taasisi hizi mbalimbali, kuna haja ya kuweka Mfumo bora wa uratibu. Sura hii inaeleza Mfumo huo wa uratibu utakaotumika pamoja na majukumu mahsusi ya kila Mdau Mkuu katika utekelezaji wa Mkakati huu.

### 4.1 Mfumo wa uratibu

Uratibu wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Wafanyakazi wa Nyumbani utafanyika kupitia Kamati ya Kitaalam ambayo itajumuisha Wataalam kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu-KAM Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM - TAMISEMI); Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; Wizara ya Fedha; Wizara ya Afya; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum; Wizara ya Katiba na Sheria; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi, Ofisi ya Taifa ya Takwimu; Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Chama cha Waajiri Tanzania, Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania, Vyama vya Wafanyakazi, Mashirika ya Umoja wa Mataifa, Asasi zisizo za Kiserikali, Asasi za Kiraia, Asasi za Kijamii za Biashara, Vyuo Vikuu na Asasi za Kidini.

Kamati itakutana kila baada ya miezi mitatu (robo mwaka) ili kufuatilia utekelezaji wa Mkakati, kutathmini changamoto zinazojitokeza na kushirikiana katika kubadilishana uzoefu na mafanikio yaliyopatikana.

### 4.2 Majukumu na wajibu wa wadau katika Kamati ya Kitaalam

Majukumu mahsusi ya Kamati ya Kitaalamu ni kama ifuatavyo:

**i.** Kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mkakati katika Halmashauri zote za Mkoa husika.
**ii.** Kutoa ushauri wa kitaalamu na msaada wa kiufundi kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa Mkakati.
**iii.** Kukusanya na kuandaa taarifa za utekelezaji katika ngazi ya Mkoa.
**iv.** Kutoa elimu kwa wadau kuhusu Mkakati wa Taifa wa Wafanyakazi wa Nyumbani.

Kanda na Maafisa wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi wa Kanda watawajibika kukusanya taarifa kutoka kwa Sekretarieti za Mikoa na wadau wengine wa Wafanyakazi wa Nyumbani, kisha kuziwasilisha Ofisini kwa ajili ya kuchakata na kufuatilia utekelezaji kitaifa.

**Jedwali Na. 3: Uanachama na Wadau katika Miundo ya Uratibu**

| Kamati | Mikutano/Mripoti | Wadau |
|---|---|---|
| Kamati za Kitaalamu | Kila robo mwaka | Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi Ajira na Mahusiano (OWM - KAM), Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM -TAMISEM Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; Wizara ya Fedha; Wizara ya Afya; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum; Wizara ya Katiba na Sheria; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA), Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), Ofisi ya Taifa ya Takwimu; Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), Vyama vya Wafanyakazi, Mashirika ya Umoja wa Mataifa, Asasi zisizo za Kiserikali, Asasi za Kiraia, Asasi za Kijamii za Biashara, Vyuo Vikuu na Asasi za Kidini. . |

# SURA YA TANO

# UFUATILIAJI NA TATHMINI

## 5.0 Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini

Ufuatiliaji na tathmini ni nyenzo muhimu katika kufuatilia utekelezaji wa Mkakati kwa Waajiri ili kujiridhisha na uzingatiaji wa viwango vya kazi ikiwemo kutoa Mikataba ya ajira, kulipa mshahara unaokidhi matakwa ya Sheria pamoja na uboreshaji wa mazingira ya kazi. Wajibu wa jumla wa ufuatiliaji upo chini ya Wizara yenye dhamana ya Masuala ya Kazi na Ajira, ambayo ndiyo Taasisi ya uratibu wa utekelezaji wa Mkakati huu.

Ufuatiliaji utafanyika kupitia Kaguzi za Kazi na Ziara za Usimamizi. Vilevile, tathmini itafanyika kupitia Taarifa za utekelezaji zitakazoandaliwa.

### 5.1 Viashiria muhimu vya Kiutendaji

Ufuatiliaji na tathmini ya Mkakati wa Wafanyakazi wa Nyumbani ni hatua muhimu katika kuhakikisha utekelezaji wake unafanikisha malengo yaliyokusudiwa. Viashiria Muhimu vya Kiutendaji na matokeo tarajiwa vitatumika kufuatilia maendeleo na mafanikio ya Mkakati katika hatua mbalimbali.

### 5.2 Uwasilishaji wa Taarifa na Uwajibikaji

Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mkakati utafanyika kwa msingi wa robo mwaka, nusu mwaka na kila mwaka ili kufuatilia hali ya utekelezaji. Ripoti zitakazotayarishwa kupitia mchakato wa ufuatiliaji na tathmini zitatumika kuwapa wadau taarifa sahihi na kwa wakati, pamoja na kuweka Mifumo ya uwajibikaji kwa ajili ya utekelezaji wenye ufanisi. Aidha, Mkakati huu utapitiwa upya baada ya kipindi cha miaka mitatu au mapema zaidi endapo kutatokea sababu maalum.

# SURA YA SITA

## 6.0 HITIMISHO

Mkakati wa Kitaifa wa Wafanyakazi wa Nyumbani nchini unawakilisha mbinu jumuishi na ya kina katika kuhakikisha haki, ustawi na utambuzi wa kitaaluma kwa Wafanyakazi wa Nyumbani. Kupitia kuimarisha Mifumo ya Kisheria, kupanua wigo wa Hifadhi ya Kijamii, kuhakikisha mazingira bora ya kazi na kuendeleza ujuzi wa Wafanyakazi, Mkakati huu umeweka msingi madhubuti wa kulinda maslahi ya Wafanyakazi wa Nyumbani. Aidha, Malengo mahsusi kwa ajili ya Wafanyakazi wa Nyumbani Wahamiaji, Kampeni za kuongeza uelewa, pamoja na kuweka mipaka ya wazi kuhusu haki na wajibu, vinahakikisha kwamba kila mdau kuanzia Taasisi za Serikali, Waajiri hadi Mashirika ya Wafanyakazi wanashiriki kikamilifu katika kujenga mazingira salama, yenye usawa na yenye kuheshimu utu kwa Wafanyakazi wa Nyumbani.

Mkakati huu, pia unaweka mkazo katika kuhitaji uwezo imara wa Kitaasisi, ushirikiano wa wadau mbalimbali na Mifumo madhubuti ya ufuatiliaji na tathmini. Kupitia malengo yaliyowekwa na viashiria vinavyopimika, Mkakati huu, haufanyi kazi tu kama ramani ya mabadiliko ya Kisera, bali pia kama ahadi ya mageuzi ya Sekta ya Kazi za Nyumbani nchini. Hatimaye, Mkakati huu unafungua njia ya maendeleo endelevu, kwa kuhakikisha Wafanyakazi wa Nyumbani wanakuwa na uwezo wa kuchangia kwa Tija katika ukuaji wa Taifa, huku wakifurahia Kazi zenye Staha.

**Kiambatisho cha 1: JEDWALI LA MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

| Nguzo ya Mkakati / Masuala muhimu | Matokeo tarajiwa | Malengo ya kimkakati | Shughuli | Matokeo | Viashiria muhimu vya kiutendaji | Watekelezaji muhimu | Taasisi itakayosimamia |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Nguzo ya 1: Mazingira ya kazi yenye staha** | Kuboreka kwa mazingira ya kazi kwa Wafanyakazi wa Nyumbani. | Mfumo wa Kima cha Chini cha mshahara kwa Wafanyakazi wa Nyumbani uwe umeanza kutumika<br><br>Mikataba ya viwango vya ajira kwa Wafanyakazi wa Nyumbani iwe imeandaliwa na kutekelezwa | Kuandaa warsha wadau wa Utatu (Serikali, Waajiri na Wafanyakazi) kwa ajili ya kuandaa Mikataba ya Viwango vya ajira kwa ajili ya Wafanyakazi wa Nyumbani.<br><br>Kufanya Programu za uhamasishaji kwa Waajiri kila robo mwaka. | Kima cha Chini cha mshahara kwa Wafanyakazi wa Nyumbani kimewekwa rasmi. | Idadi ya Wafanyakazi wa Nyumbani wanaopokea mshahara usiopungua Kima cha Chini kilichowekwa. | Ofisi ya Waziri Mkuu –TAMISEMI, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Katiba na Sheria, Chama cha Waajiri Tanzania Vyama vya Wafanyakazi, ILO. Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia, Wadau wa Kijamii na Kiuchumi, | OWM-KAM |
| | | | Kuwezesha Ukaguzi wa pamoja wa kazi kati ya Serikali za Mitaa na vyombo vya ajira. | Fomu mahsusi ya Ukaguzi wa Kazi (Checklist) kwa Wafanyakazi wa Nyumbani ipo na inatumika. | Uwiano wa Waajiri wanaozingatia Viwango vya Kazi dhidi ya wale wasiozingatia (compliance vs non-compliance). | | |

| Nguzo ya Mkakati / Masuala muhimu | Matokeo tarajiwa | Malengo ya kimkakati | Shughuli | Matokeo | Viashiria muhimu vya kiutendaji | Watekelezaji muhimu | Taasisi itakayosimamia |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kufanya Mapitio ya Mwongozo wa Kaguzi za Kazi ili kujumuisha Fomu mahsusi ya Ukaguzi (Checklist) kwa Wafanyakazi wa Nyumbani<br><br>Kufanya Mapitio ya Kima cha Chini cha Mshahara.<br><br>Kuelimisha Waajiri kuhusu haki za Watu Wenye Ulemavu | Mikataba ya viwango vya ajira kwa Wafanyakazi wa Nyumbani | Idadi ya waajiri walioelimishwa kuhusu haki za Watu Wenye Ulemavu. | | |
| **Nguzo ya 2: Hifadhi ya Jamii na Ustawi** | Kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma za Hifadhi ya Jamii na Mafao ya ustawi kwa Wafanyakazi wa Nyumbani. | Uandikishaji wa Wafanyakazi wa Nyumbani katika Mifumo ya Hifadhi ya Jamii kuongezeka kwa asilimia 2 ifikapo mwaka | Kuwezesha usajili wa Wafanyakazi wa Nyumbani katika mifuko ya Hifadhi ya Jamii. | Wafanyakazi wa Nyumbani wamesajiliwa katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. | Idadi ya Wafanyakazi wa Nyumbani waliosajiliwa katika Mifumo ya Hifadhi ya Jamii. | Wizara ya Afya, Wizara ya Fedha, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mamlaka za | OWM-KAM |
| | | | Kufanya uchambuzi wa | Uwepo wa Mfumo wa | | | |

| Nguzo ya Mkakati / Masuala muhimu | Matokeo tarajiwa | Malengo ya kimkakati | Shughuli | Matokeo | Viashiria muhimu vya kiutendaji | Watekelezaji muhimu | Taasisi itakayosimamia |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2030.<br><br>Kuongezeka kwa uelewa wa Wafanyakazi wa Nyumbani kuhusu hifadhi ya jamii. | hali halisi kuhusu ushiriki wa Wafanyakazi wa Nyumbani katika Mifumo ya Hifadhi ya Jamii. | gharama nafuu katika Hifadhi ya Jamii | | Hifadhi ya Jamii, Vyama vya Wafanyakazi. | |
| | | | Kufanya mapitio ya Mfumo wa Fidia kwa Wafanyakazi ili kujumuisha Waajiri wa Wafanyakazi wa Nyumbani. | Wafanyakazi wa Nyumbani wananufaika na Mfuko wa Fidia kwa madhara au majeraha yanayotokea wakati wa utekelezaji wa kazi zao. | | | |
| **Nguzo ya 3: Ulinzi wa Kisheria, uelewa wa haki na wajibu** | Kuimarika kwa ulinzi wa Kisheria na utekelezaji wa haki za kikazi kwa Wafanyakazi wa Nyumbani. | Upatikanaji wa huduma za msaada wa Kisheria zinazowalenga mahsusi Wafanyakazi wa Nyumbani ifikapo 2030. | Kufanya Maboresho ya Sheria za kazi ili kujuimuisha masuala ya Wafanyakazi wa Nyumbani | Maboresho katika sheria za kazi kwa Wafanyakazi wa Nyumbani yamefanyika | Kuanza kutumika kwa marekebisho ya Sheria | Wizara ya Katiba na Sheria, Vyama vya Wafanyakazi, Asasi za Kiraia, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi, Maafisa Kazi. | OWN- KAM |
| | | | Kufanya Kampeni za uhamasishaji kote nchini | Mazingira bora ya kazi yaliyo rafiki na yenye kulinda haki. | Idadi ya Waajiri waliopata uhamasishaji kuhusu haki za | | |

| Nguzo ya Mkakati / Masuala muhimu | Matokeo tarajiwa | Malengo ya kimkakati | Shughuli | Matokeo | Viashiria muhimu vya kiutendaji | Watekelezaji muhimu | Taasisi itakayosimamia |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | kuhusu haki za Wafanyakazi. | | Wafanyakazi wa Nyumbani. | | |
| | | | Kuandaa kanuni maalum za maadili ya utendaji au kanuni za udhibiti kwa ajili ya Wafanyakazi wa Nyumbani. | Mifumo ya kufuatilia utekelezaji wa Sheria za Kazi. | Idadi ya Maagizo ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Sheria yaliyotolewa. | | |
| | | Uwepo wa mfumo wa kushughulikia Migogoro ya Kazi na unaoweza kufikiwa kwa urahisi na Wafanyakazi wa Nyumbani wakiwemo Wenye Ulemavu pamoja na Waajiri wao, bila vikwazo vya gharama, | Kutoa huduma za Kliniki inayotembea kwa ajili ya utatuzi wa Migogoro ya Kazi. | Utoaji wa taarifa muhimu kuhusu haki za Wafanyakazi. | Idadi ya Malalamiko yaliyopelekwa OWM-KAM<br><br>Idadi ya Migogoro ya Kazi iliyowasilishwa kwa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi. | | |

| **Nguzo ya Mkakati / Masuala muhimu** | **Matokeo tarajiwa** | **Malengo ya kimkakati** | **Shughuli** | **Matokeo** | **Viashiria muhimu vya kiutendaji** | **Watekelezaji muhimu** | **Taasisi itakayosimamia** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | umbali au urasimu ifikapo mwaka 2030. | | | | | |
| **Nguzo ya 4: Kuendeleza ujuzi na ukuaji kitaaluma** | Kuimarika kwa umahiri wa Wafanyakazi wa Nyumbani na maendeleo ya kazi zao. | Programu za Mafunzo mahsusi ziwe zimeandaliwa na kutekelezwa ifikapo mwaka 2030. | Kuanzisha Programu za Mafunzo ya Ufundi Stadi, Kozi za Cheti na Mafunzo ya stadi za maisha.<br><br>Kuimarisha uwezo wa Maafisa Kazi na Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi kuhusu mageuzi ya Sheria za Kazi. | Kuongezeka kwa upatikanaji wa Programu za kukuza ujuzi na utambuzi kwa umahiri wa Wafanyakazi wa Nyumbani. | Idadi ya Programu zilizoundwa za Mafunzo kwa Wafanyakazi wa Nyumbani. | Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), Vyuo Vikuu, Vyama vya Wafanyakazi. | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. |
| | | | Kufanya ufuatiliaji wa wahitimu wa mafunzo ya Kazi za Nyumbani (tracer study). | Taarifa ya ufuatiliaji wa wahitimu wa mafunzo (tracer report). | Idadi ya Wafanyakazi wa Nyumbani waliomaliza Mafunzo ya ujuzi kwa mafanikio wakiwemo Wenye Ulemavu. | | |

| Nguzo ya Mkakati / Masuala muhimu | Matokeo tarajiwa | Malengo ya kimkakati | Shughuli | Matokeo | Viashiria muhimu vya kiutendaji | Watekelezaji muhimu | Taasisi itakayosimamia |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kuandaa na kutekeleza Programu za kutambua ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi kwa kushirikiana na vituo vya VETA. | | | | |
| **Nguzo ya 5: Vyama vya Wafanyakazi na uchechemuzi**. | Kuimarika kwa ushiriki wa Wafanyakazi wa Nyumbani katika Vyama vya Wafanyakazi. | Kuhakikisha Wafanyakazi wa Nyumbani wanakuwa na uhuru wa kujiunga na Vyama vya Wafanyakazi. | Kuimarisha ulinganifu na ujumuishaji wa Mifumo ya usimamizi wa taarifa za Wafanyakazi wa Nyumbani. | Mifumo inayosomana ya usimamizi wa taarifa na Takwimu. | Kupungua kwa utofauti/kukinzana kwa Takwimu. | Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), Vyama vya Wafanyakazi, Asasi za Kiraia, Asasi za Kijamii. | OWM-KAM |
| | | | Kuandaa mipango ya utekelezaji ya kila mwaka ya uchechemuzi.<br><br>Kuandaa mpango wa uhamasishaji wa rasilimali. | Mipango ya utekelezaji ya kila mwaka imeandaliwa. | Idadi ya Wafanyakazi wa Nyumbani waliojiunga na Vyama vya Wafanyakazi. | | |

| Nguzo ya Mkakati / Masuala muhimu | Matokeo tarajiwa | Malengo ya kimkakati | Shughuli | Matokeo | Viashiria muhimu vya kiutendaji | Watekelezaji muhimu | Taasisi itakayosimamia |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kuratibu ushirikiano kati ya Taasisi mbalimbali ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa Sera kupitia mikutano ya uratibu iliyo rasmi na vikosi kazi. | Vikao vya vikosi kazi vinafanyika. | Idadi ya vikao vya vikosi kazi vilivyofanyika. | | |
| | | | Kuwezesha Kampeni za utetezi na uhamasishaji kwa ajili ya Wafanyakazi wa Nyumbani. | Kuanza kufanya kazi kwa Mifumo ya usaidizi kwa Wafanyakazi wa Nyumbani. | Idadi ya majukwaa ya kidijitali yaliyoanzishwa na yanafanya kazi.<br>Idadi ya Kampeni za utetezi zilizoanzishwa na kutekelezwa. | | |
| **Nguzo ya 6: Ulinzi wa Wafanyakazi wa Nyumbani Wahamiaji** | Kuimarika kwa ulinzi wa Wafanyakazi wa Nyumbani Wahamiaji. | Kuimarisha haki za Wafanyakazi wa Nyumbani Wahamiaji ifikapo mwaka 2030. | Kuandaa na kutekeleza Mifumo ya kuwalinda Wafanyakazi wa Nyumbani Wahamiaji, ikiwa ni pamoja na taratibu salama za uhamaji, nyaraka halali | Kuimarishwa kwa Mifumo ya ulinzi wa Wafanyakazi wa Nyumbani Wahamiaji. | Kiwango cha ufuatiliaji wa utekelezaji wa Sheria za Kazi. | Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya mambo ya Nje, Ubalozi, Mashirika ya Kimataifa | OWM-KAM |

| Nguzo ya Mkakati / Masuala muhimu | Matokeo tarajiwa | Malengo ya kimkakati | Shughuli | Matokeo | Viashiria muhimu vya kiutendaji | Watekelezaji muhimu | Taasisi itakayosimamia |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | za Kisheria na msaada wa Kidiplomasia kwa Wafanyakazi walioko nje ya nchi. | | | (Shirika la Kazi Duniani, Taasisi nyingine za Umoja wa Mataifa), Asasi za Kiraia. | |
| | | | Kuwezesha ushirikiano wa mipakani ili kuhakikisha ulinzi wa Wafanyakazi wa Nyumbani Wahamiaji na kuhimiza ajira zinazozingatia haki katika ngazi ya Kimataifa. | | Idadi ya Mikataba au makubaliano ya uwili (Bilateral Agreements/MoUs) iliyotiwa saini. | | |
| | | | Kutoa mafunzo ya awali kabla ya kusafiri kwa Wafanyakazi wa Nyumbani. | Kufanyika kwa Mafunzo ya awali kabla ya kusafiri. | Idadi ya Wafanyakazi wa Nyumbani waliopata Mafunzo. | | |
| | | | Kuendesha Mafunzo ya kujenga uwezo | Kuhamasika kwa Wadau wa Wafanyakazi wa | Idadi ya Malalamiko ya Wafanyakazi | | |

| Nguzo ya Mkakati / Masuala muhimu | Matokeo tarajiwa | Malengo ya kimkakati | Shughuli | Matokeo | Viashiria muhimu vya kiutendaji | Watekelezaji muhimu | Taasisi itakayosimamia |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | mipakani ili kuhakikisha ulinzi wa Wafanyakazi wa Nyumbani Wahamiaji na kuhimiza ajira zinazozingatia haki katika ngazi ya Kimataifa. | | uwili (Bilateral Agreements/MoUs) iliyotiwa saini. | | |
| | | | Kutoa mafunzo ya awali kabla ya kusafiri kwa Wafanyakazi wa Nyumbani. | Kufanyika kwa Mafunzo ya awali kabla ya kusafiri. | Idadi ya Wafanyakazi wa Nyumbani waliopata Mafunzo. | | |
| | | | Kuendesha Mafunzo ya kujenga uwezo kwa wadau wanaohusika na haki za Wafanyakazi wa Nyumbani Wahamiaji. | Kuhamasika kwa Wadau wa Wafanyakazi wa Nyumbani kuhusu haki za Wafanyakazi wa Nyumbani. | Idadi ya Malalamiko ya Wafanyakazi Wahamiaji yaliyoripotiwa katika Ubalozi. | | |

Mkakati umeandaliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO)

Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira na Mahusiano

Mtaa wa Kazi, Mji wa Serikali, Mtumba

S.L.P. 2890 Dodoma, Tanzania

www.kazi.go.tz